MAONYESHO YA "SWAHILI FASHION WEEK & AWARDS" KWA MWAKA WA 2020 YAZINDULIWA RASMI

MAONYESHO YA 13 YA "SWAHILI FASHION WEEK" KUFANYIKA MNAMO TAREHE 4,5 &6 DESEMBA

WABUNIFU 45 KUONYESHA VIPAJI VYAO KWENYE JUKWAA HILO DAR ES SALAAM

Jukwaa kubwa la maonyesho ya mavazi Afrika Mashariki na Kati la *"Swahili Fashion Week & awards"*(#SFW2020) limepanga kufanya maonyesho yake tarehe 4,5 & 6 Desemba mwaka huu, Hoteli ya Serena Jijini Dar es Salaam na linatarajia kuleta pamoja wabunifu wapatao 45 kutoka nchi za Afrika Mashariki na kwingineko ulimwenguni. Ikiwa imejijengea mafanikio makubwa kwenye maonyesho yake miaka iliyopita, jukwaa la *"Swahili Fashion Week & awards"* bado linaongoza kwa umahiri katika tasnia hii ya ubunifu wa mavazi.

Muasisi wa *"Swahili Fashion Week & awards"* Mustafa Hassanali ana matumaini ya kuimarisha msingi wa ubora wa jukwaa hilo na kwa shauku kubwa anasema, "Mwaka 2020 umekuwa na changamoto nyingi sana kiuchumi, mnamo mwezi Aprili tulipokua kwenye hatua za mwanzo za maandalizi ya jukwaa hili la mwaka huu, tulikua na wasiwasi mkubwa juu ya uwezekano wa kufanyika kwa maonyesho haya, pamoja na chanagamoto zinginezo zikiwemo janga la homa ya Korona (Covid 19) wabunifu zaidi ya arobaini na tano (45) wanatarajiwa kuonyesha ubunifu wao kwenye jukwaa la mwaka huu. Hii ni kwa sababu ya hatua zenye tija na chanya zilichichukuliwa na kiongozi wetu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. John Pombe Magufuli katika kuthibiti janga hilo."
Mustafa anaongeza, "lengo la kuendeleza tasnia ya ubunifu Afrika bado linabaki mstari wa mbele, kwa kupitia jukwaa hili na mtandao wake mkubwa wa vyombo vya habari, watumiaji wa bidhaa za ubunifu wa Tanzania, Afrika na ulimwengu kwa ujumla sasa wataweza kuona mbadala wa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje, na kwa wakati wote tumekua tukitilia mkazo thamani ya bidhaa za ubunifu za Afrika kwa kuhamasisha adhana ya "made in Africa" nakutengeneza bidhaa zenye hadhi ya kimataifa kwa misingi ya Kiafrika."
Maonyesho haya ya wa kumi na tatu(13) ya *"Swahili Fashion Week & awards"* yataendelea kuwa kioo kwa maonyesho mengine ya mavazi Afrika kwa wabunifu wa Kitanzania, ukanda wa Afrika Mashariki hata wale wa kimataifa kwa mvuto na mandhari yake ya kipekee inayoendana na kauli mbiu ya jukwaa ya Tambua Kinachoipendezesha Afrika "Discover What Makes Africa Beautiful."

"Tunauhamasisha umma wa Watanzania kupenda kuvaa mavazi yaliyobuniwa na wabunifu wa hapa Tanzania (Made in Tanzania). Kwa kufanya hivyo tunakuza vipaji vyao na kuwafanya siku moja kutambulika kama wabunifu wakubwa Ulimwenguni. Upendo unaanzia nyumbani na ndiyo dhumuni la kufanya haya..kukuza tasnia hii ya ubunifu"Aliongeza Hassanali.
Jukwaa pia linawahimiza wabunifu wachanga kutumia jukwaa hili kama hatua moja wapo kwenye safari yao ya kukuza vipaji vyao vya ubunifu. Kwa mara nyingine tena kutakua na shindano la wabunifu chipukizi linalojulikana kama "Washington Benbella Emerging Designers Competition" ambapo wabunifu tisa(9) wanatarajiwa kuonyesha umahiri wao kwenye ubunifu kupitia jukwaa hili.
Akizungumza wakati wa uzinduzi huo Balozi wa Italia hapa Nchini Mh. Roberto Mengoni alisema, "kwa kipindi cha miaka sita(6) mfululizo tumekua tukishirikiana na jukwaa hili la Swahili Fashion Week & Awards kwenye maonyesho yao, na kwa mara nyingine tena mwaka huu tunaungana nao kufanikisha maonyesho haya ya kumi na tatu. Tumejionea ukuaji na maendeleo makubwa katika tasnia hii ya mitindo hapa Tanzania na ni heshima kwetu kuwa sehemu ya ukuaji na maendeleo hayo. Ubalozi pia umefanikisha ushiriki wa mbunifu Maria Laurenza kutoka Italia atakayeonyesha

ubunifu wake kwenye jukwaa hili pamoja na kuendesha warsha kwa wabunifu wenzake kupitia jukwaa hili."
Kwa kipindi cha miaka kumi na mbili iliyopita (12) Swahili Fashion Week imejizolea Umaarufu mkubwa na kujulikana kama jukwaa kubwa la maonyesho mavazi katika ukanda wa Afrika Mashariki na kati likitoa nafasi kwa wabunifu kutoka Nchi zinazozungumza lugha ya kiswahili na kwingineko Afrika, kuonyesha vipaji vyao na kupanua wigo wa masoko yao.

Katibu mtendaji wa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) Bw. Godfrey Mngereza alinukuliwa akisema, "Sekta ya mavazi kwa ujumla imekua na mchango mkubwa katika uchangiaji wa pato la Taifa, nah ii ni kutokana na matumizi mazuri kabisa ya zao la pamba, sekta ya mavazi imekua na muitikio chanya juu ya sera ya Tanzania ya viwanda, na unapozungumzia ukuaji wa viwanda, moja kwa moja huwezi kuacha kuzungumzia ukuaji wa sekta hii ya mavazi. Na kwa kufahamu hilo, sisi kama Baraza daima tumekua mstari wa mbele kuhakikisha tunakua na msaada wenye tija kwa wabunifu pamoja na wadau mbalimbali wa sekta hii ya ubunifu hapa nchini. Napenda pia kuwapongeza kwa uamuzi wao wa kubuni na kutengeneza barakoa za vitambaa vilivyozalishwa hapa Tanzania, kwa kufanya hivyo waliihakikishia jamii usalama dhidi ya janga la Korona. Tunapenda zaidi na zaidi kuamsha mwitiko na kupenda kutumia bidhaa za kitanzania ili kuhakikisha ukuaji wa kwetu kama taifa na kuleta maendeleo yenye tija.
"Kwa hakika Jukwaa hili la Swahili Fashion Week limejiweka katika nafasi nzuri kwenye ukuaji na maendeleo ya tansia ya ubunifu wa mavazi hapa nchini na kwingineko Afrika. Ni furaha kutangaza rasmi kwamba jukwaa litasheherekea manyesho yake ya kumi na tatu tarehe 4 – 6 Desemba."
"Kwa namna ya kipekee tunatambua na kupongeza kazi nzuri iliyofanywa na viongozi wetu kuhakikisha usalama hapa Nchini dhidi ya janga la homa ya Korona (Covid 19) na hivyo maonyesho yatafanyila kwa amani na usalama. Tunaamini kwamba hili ni jukwaa lililojikita kwenye kuibua na kukuza vipaji vya ubunifu hapa nchini." Aliongeza Mngereza.

Huu ni mwaka wa pili hoteli ya Serena Dar Es Salaam inakua mwenyeji wa maonyesho hayo na wanayo shauku kubwa ya kupokea na kuhudumia wadau wote wa tasnia hiyo ubunifu, "Napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza sana waandaaji wa Swahili fashion week na kwa namna ya pekee ya pekee Muasisi ndugu Hassanali kwa jitihada zao katika kuhakikisha uendeshaji wa jukwaa hili unakua wenye mafanikio, sisi kama hoteli ya Serena Dar Es Salam kwa mara nyingine tena tunayo furaha kuwa mwenyeji wa maonyesho haya. Hoteli za Serena ndizo hoteli zinazopatikana kwa wigo moana zaidi katika ukanda huu wa Afrika Mashariki, hivyo tumeona ni vyema kuungana na jukwaaa kubwa la mavazi Afrika Mashariki na kati kufanikisha maonyesho haya na tunawakaribisha sana hoteli za Serena." Alisema Seraphin Lusala, Meneja wa mauzo wa Serena hoteli Dar Es Salaam.
"Napenda pia kutoa rai kwa wabunifu pamoja na wadau wengine kutumia nafasi hii na kufanyamambo kadha wa kadha hususan maeneo yale ambayo Serena imewekeza kutoa huduma ya malazi na sisi tupo tayari kuwaunga mkono kwenye shughuli zao." Aliongeza Seraphin.

Katika Maonyesho ya mwaka huu pamoja na maonyesho ya mavazi(runway) yatakayofanyika kila siku kwa kipindi cha siku tatu mfululizo kuanzia saa 2.30 usiku, kutakua na Bazaar ambapo wabunifu wataonyesha na kuuza bidhaa zao mbalimbali kuanzia saa 1.00 usiku. Sambamba na hilo tutasheherekea na kutambua mchango wa wadau mbalimbali kwenye tasnia ya ubunifu ambapo tuzo kutoka vipengele 26 zitatolewa. "Mwaka huu tumeongeza vipengele vipya kwenye tuzo zetu ambavyo ni ubunifu bora wa mavazi ya video ya muziki pamoja na ubunifu bora wa mavazi ya filamu. Tuzo za Swahili Fashion Week zinaletwa kwenu na Green Telecom na kusimamiwa na Nexia SJ" alisema Hassanali.

Swahili Fashion Week & Awards 2020 imejizatiti kwenye matumizi teknolojia ya hali ya juu kwa kuonyesha umahiri wa uandaaji katika kipindi cha siku hizo za mitindo na urembo, pamoja na

miondoko ya wanamitindo waliojiandaa vizuri jambo litakaloendelea kuiweka Tanzania kwenye kilele cha ubora. Tanzania, Haisahauliki (Tanzania, Unforgetable).

Swahili Fashion Week Inaandaliwa na kuratibiwana 361 Degrees Africa Ltd, wenyeji wakiwa ni Hoteli ya Serena Dar Es Salaam na inadhaminiwa na UbaloziWa Italia Tanzania, Grey Goose, Hugo Domingo, Image Masters, Asila's Make Up, Nexia SJ, Green Telecom, Epidor, Events lites, Maasai Watchers, Spik N' Span, Image Masters, Khimji's, A1 Outdoor, Fashion Association of Tanzania pamoja na Baraza La Sanaa La Taifa(BASATA).

Wabunifu katika jukwaa la mwaka huu ni:
LUNDI & SONS | ENOFITS | ANETELLA | CHUWA FASHION | ASHUBIRA DESIGNS |MILLY'Z | DD_CRAFTS | MARIEPRINTS | EK-AN-TIK | TWIGASMODE | MARTIN KADINDA | BY JV'S | MATT DESIGNS | ZADO FASHION | NKIPOSH DESIGNS | NYUZI CAD | KIKI'S FASHION | KATTY COLLECTION | LEVRA WITH CULTURE | THE OUTFIT BRAND | HUSSEYN AWADH | SHAHBAAZ SAYED | NIDA TEXTILES MILLS(T)LTD | UCOCO BRAND | SUKRA SALAH | AFRICAN ATTIRE FOR ALL | TEXTURE BEAUTY SAON | JK DESIGNS | RAY PLAN | MABINTI CENTRE | ZUH FASHION | T-NGAZY | DAPPER LUQ COLLECTION | IRADA STYLE | MKWANDULE`SON | CLAVON LEONARD | NAA LAMLEY KOUTURE | MORREZ FASHION | IMAQULATEDESIGNS | MAHAUMES DESIGNS | AFRIPOSH DESIGNS | BANSRI.M. | ENJIMAASAI | T.E.FASHION | MARIA LAURENZIA

Kuhusu Swahili Fashion Week:
Swahili Fashion Week Ni Jukwaa kubwa la maonyesho ya mavazi Afrika Mashariki na kati linalotoa fursa kwa wabunifu wa mavazi kutoka nchi zinazozungumza lugha ya Kiswahili na kwingineko Afrika kuonesha vipaji vyao nakupanua wigo wao wa masoko.
Dhamira kuu ni kudhihirisha kwamba ubunifu wa mavazi ni shughuli inayoweza kumwingizia mtu kipato sambamba na kuhamamisha dhana ya Made in Africa.
Maonyesho ya Swahili Fashion Week yalianzishwa mwaka 2008 na muasisi wake Mustafa Hassanali.
Mwaka huu wa 2020 yakiwa ni maonyesho yake ya 13.

Maulizo kwa Vyombo vya habari, Wasiliana na Amina Lweno +255 676 335 537

Barua Pepe:
media@swahilifashionweek.com